

SERIKALI YA AWAMU YA NNE

1. Serikali ya awamu ya nne chini ya Rais Kikwete,
Tuiunge mkono wazalendo, Tanzania (wazalendo),
Tunahitaji mapinduzi, chini ya vyama vilavyo hai
Vyenye misingi na katiba.

Rais wetu Kikwete Baba,

Uishike serikali baba uingoze (uiongoze)

Taifa letu lisonge mbele (lisonge mbele)

Safari yetu ni ndefu sana uingoze (uingoze)

Tanzania twakutegemea (Tegemea)

Shirikiana nae Lowasa na mawaziri (na mawaziri)

Kari zako heri na baraka (heko baba)

Bunge lako toka visiwani na huku bara

(Latuongoza)

Hongera Samweli Sita baba (Na wabunge)

(Taifa letu linahitaji utendaji kazi)

Utendaji kazi kwa haki na uaminifu

Tuheshimu na kutunza maadili ya kazi zetu

Watazania kazi imeanza (Kazi imeanza)

Kazi kazi (Kikwete baba)

Shika,shika shika, ufagio wa chuma

(Na Lowasa) Shika, shika ufagio wa chuma

(Mawaziri) Shika shika shika ufagio wa chuma

(Akina mama wote vibwebwe ufagio wa chuma)

Tushike, tushike shike ufagio wa chuma

(mtupe na sisi watoto ufagio wa chuma)

Tushike, tushike shike ufagio wa chuma

(wazalendo wote tushike ufagio wa chuma)

Tushike, tushike shike ufagio wa chuma

(Tuzifagie fagie ofisi zetu) ziwe safi

Huduma zetu ofisini ziwe safi – na za haki

Pia tufagie mashirika ya uma – yawe safi

Hujuma wizi ulanguzi pia hongo – tuvizike

Mahakama polisi na gereza – pawe safi

Leseni na njia zote za kiuchumi – ziheshimiwe
Usajili wa vyama vyote vya saisa – uwe huru
Huduma za hospital na za elimu – ziwe safi
Ufagio wa chuma usafishe pote – pawe safi
(Wazalendo) PCB ndich chombo,
Hakijali cheo,wala jina,kupamabana na ulaji rushwa

2.Jukumu la kuendeleza na kuingoza nchi yetu,
ni wajibu wa kila mzalelendo Tanzania
(Wazalendo) Tufanye kazi kwa bidii
Tulikwamue Taifa letu litokane na umaskini
Rais wetu Kikwete baba
Ameitangaza vita kali na ya kdumu (Na ya
kudumu)
Tuwajibike watanzania (Tanzania)
Ubadhirifu, dhuluma, rushwa, havitakwisha
(havitakwisha)
Kwa kuvilaani peke yake (peke yake)
Uongozi wako – kiuchumi mabadiliko(mabadiliko)
Tanzania na Afrika yote (twayajua)
Ushirikiano Taifa na kimatifa (hongera baba)
Heko Ali Shein we makamu (wazalendo)

(Taifa letu linahitaji utendaji kazi)
Utendaji kazi kwa haki na uaminifu
Tuheshimu na kutunza maadili ya kazi zetu
Watazania kazi imeanza (Kazi imeanza)
Kazi kazi (Kikwete baba)
Shika,shika shika, ufagio wa chuma
(Na Lowasa) Shika, shika ufagio wa chuma
(Mawaziri) Shika shika shika ufagio wa chuma
(Akina mama wote vibwebwe ufagio wa chuma)
Tushike, tushike shike ufagio wa chuma
(mtupe na sisi watoto ufagio wa chuma)
Tushike, tushike shike ufagio wa chuma
(wazalendo wote tushike ufagio wa chuma)

Tushike, tushike shike ufagio wa chuma
(Tuzifagie fagie ofisi zetu) ziwe safi

Huduma zetu ofisini ziwe safi – na za haki
Pia tufagie mashirika ya uma – yawe safi
Hujuma wizi ulanguzi pia hongo – tuvizike
Mahakama polisi na gerezani – pawe safi
Leseni na njia zote za kiuchumi – ziheshimiwe
Usajili wa vyama vyote vya saisa – uwe huru
Huduma za hospital na za elimu – ziwe safi
Ufagio wa chuma usafishe pote – pawe safi
(Wazalendo) PCB ndich chombo,
Hakijali cheo,wala jina,kupamabana na ulaji rushwa